**LEARNING BY EAR 2012**

‘

**“Wasaliti walo karibu – Hadithi inayoangazia dhulma zinazoambatana na ngono”**

**EPISODE 4: “Matokeo”**

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**
**EDITOR: Andrea Schmidt, Pendo Paul**
**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: ALLAN AT HOME WITH UNCLE JOE**

- **Joe (m, 45)**
- **Allan (m, 12)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**SCENE TWO: NURU RECOVERS IN HOSPITAL**

- **Nuru (f, 30)**
- **Dulu (m, 40)**
- **Dr. Jito (m/f, 50)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**SCENE THREE: PATO AT HOME WITH HER MOTHER SEREFA**

- **Pato (f, 16)**

- **Serefa (f, 40)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

## SCENE FOUR: ALLAN, PRECIOUS AND UNCLE JOE AT HOME

- **Allan (m, 12)**
- **Joe (m, 45)**
- **Precious (f, 30)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

## UTANGULIZI:

Hujambo na karibu katika kipindi cha **Noa bongo, Jenga maisha yako** ambacho kinaletwa kwako na Deutsche Welle. Tuko katika kipindi cha nne tukiangazia dhulma za kingono barani Afrika katika hadithi ya, **'Wasaliti walo karibu'.** Katika kipindi kilichotupa kisogo, Dulu alimpeleka haraka mkewe hospitalini. Alimkuta kalala bila fahamu kando ya kisima; alikuwa na majeraha mengi baada ya kubakwa na genge la waasi. Na katika shule ya sekondari ya Kilindi, mwanafunzi mchanga Pato alidhulumiwa kingono na Bw. Maneno, mwalimu msimamizi wa mabweni, ambaye pia ni mwalimu wake wa somo la baiolojia. Ni matukio yapi yanayotusubiri? Kaa nasi katika kipindi cha leo kwa jina la, **'Matokeo'.** Tunaanza tukiwa nyumbani kwa kijana wa miaka 10**,** Allan. Ni usiku na mamake hajarudi kutoka kazini, na amemuacha mikononi mwa mpenzi wake, Uncle Joe. Kumbuka kipindi kilichopita Uncle Joe alimpiga Allan, tena kichapo cha mbwa mwitu kuingia msikitini na kukojolea msahafu.

## SCENE ONE: ALLAN AKIWA NYUMBANI NA UNCLE JOE

1. **SFX: MUSIC PLAYING FROM FM RADIO STATION**

2. **JOE:** **(Shouts)** Allan! Nilikwambia nini kuhusu kucheza muziki kwa sauti ya juu?

3. **NO REPLY - MUSIC CONTINUES**

4. **JOE:** Allan! Ninaongea na wewe! Sikukwambia ucheze mziki kwa sauti ya chini? Haya masikio yako ni mapambo? Majirani wamekwambia wanahaja ya kusikia unachosikiliza?. … Punguza sauti! Tena sasa hivi!

**SFX: MUSIC IS TURNED DOWN BUT CONTINUES IN BACKGROUND**

5. **JOE:** Kwa vile leo umeamua kuwa bubu, nataka uende bafuNI, ukaoge, na ukalale. Unanielewa? **(Pause)** …Umenielewa?

6. **ALLAN:** **(softly and fearfully)** Ndiyo.

7. **JOE:** Ndiyo, kwa hivyo unaweza kuzungumza. Haya kwenda sasa hivi. Na uhakikishe umeoga na kutakata.

8. **MSIMULIZI:** Bwana mdogo Allan anaishi na jinamizi. Hajawahi kuona mtu katili kama mpenzi wa mamake, Uncle Joe. Lakini kwa bahati mbaya Allan hajajuwa kuwa kipigo anachopewa na Uncle ni mwanzo tu, kwani mengi yanamsubiri. Allan anafanya alivyoamuriwa, na anakwenda kuoga…

9. **SFX: SHOWER RUNNING**

10. **ALLAN:** **(singing song that previously was on radio)**

11. **SFX: CREAKING SOUND AS WHEN OLD DOOR IS OPENED**

12. **JOE:** **(excited)** Enhe, vyema, hebu tumuone huyu ni nani bafuni!

**13. ALLAN:** **(protesting)** Uncle Joe! Toka! Mimi ninaoga! Uncle Joe… unafanya nini huku? **(continues screaming)**

**14. MSIMULIZI:** Kwa Waafrika wengi, mambo ya ngono ni miiko kuzungumzia. Hayasemwi kamwe. Kina baba hawayaongei na vijana wao, kina mama pia hawayagusii na binti zao. Wengine hujifanya kama mambo haya hayatokei kamwe – mpaka linapowafika. Uncle Joe anachukua fursa hii, kumlawiti Allan. Kijana mdogo ameachiwa kumlea, lakini badala ya kumchunga Allan, anamdhulumu kingono. Kutatokea nini sasa? Punde tutayang'amua haya madhila haya… Upande mwengine wa nchi, Nuru yuko hospitalini baada ya kubakwa kinyama. Alipoteza fahamu kwa muda, na alipopata nafuu, mumewe Dulu alikuwa ubavuni mwake.

**<u>SCENE TWO: NURU AKIPATA SHUFAA HOSPITALI</u>**

**15. SFX: HOSPITAL ATMO**

**16. NURU:** **(yawning)**

**17. DULU:** Nuru, mke wangu mpendwa. Nafurahi kukuona umepata ahueni.

**18. NURU:** **(slowly coming to)** Dulu … Kumetokea nini? Kwanini niko hospitali? **(starts to weep)** Hapana…usiniambie walinifanyia hivi… sitaki kukumbuka chochote!

**19. DULU:** Usilie, Nuru. Ni sawa sasa. Uko salama ukiwa nami. Nuru, tafadhali… usilie.

**20. SFX: HOSPITAL CURTAIN DRAWN**

**21. DR. JITO:** Oh, vyema – naona Nuru umeamka. Ni… nina habari kwenu nyote.

**22. DULU:** Daktari, haiwezi kusubiri?

**23. DR. JITO:** La, samahani, haiwezi kusubiri… Nuru – kama daktari, kazi yangu kubwa ni kuwashauri wenye majeraha ya kimwili; ni habari za kipaumbele kama hizi.

**24. NURU:** Kuna nini, Daktari? Nitakufa? Sivyo?

**25. DR. JITO:** Nuru – hebu tulia. Ilikuwa vyema ulileletwa haraka hapa, lakini juu ya hayo, ni vyema…

**26. DULU:** **(shocked)** Tafadhali usiniambie wamemuambukiza virusi vya ukimwi!

**27. DR. JITO:** Tafadhali, niache nimalize. Najua huu ni wakati mgumu kwenu nyote. Lakini kama daktari, nitawaeleza kila kitu. Kama nilivyosema ni vyema kwenu nyotekuwepo hapa, ndiyo tuweze kutibu

majeraha yote. Hata hivyo, kulingana na huo udhalimu uliofanyika basi mtoto wenu mliokuwa mkitarajia ametoka.

**28. (Nuru and Dulu shocked)**

**29. DULU:** Ati! Oh la… siamini.

**30. NURU:** **(weeping)** Samahani, Dulu… nilijaribu, nilifanya niwezavyo… walikuwa wengi na wenye nguvu.

**31. DR. JITO:** Tafadhali, jipe moyo. Najuwa huu ni wakati mgumu. Tushukuru kwamba Nuru yu hai. Tutamfanyia vipimo vya virusi vya ukimwi miezi mitatu baada ya tukio hili. Tutafanya tuwezavyo ili uponyaji uwe kamili.

**32. DULU:** **(bitterly)** La! Mtoto wetu… mtoto wetu maskini.

**33. NURU:** Dulu, tafadhali usinichukie! Sio kupenda kwangu!

**34. DULU:** **(still bitter)** Kwanini sisi? Kwanini mimi? Kwanini sasa? Arrrgh – hao wanyama waliokutendea haya nitawamaliza!

**35. DR. JITO:** **(coughs to interrupt)** Bwana… mkeo amekumbwa na matokeo magumu ya kimwili na hisia. Jukumu letu ni kumtibu, lakini anafaa pia umtafutie huduma

ya ushauri nasaha. Unahitaji upate huduma za mtaalamu wa akili. **(whispers to Dulu)** Lakini Bwana, kitu zaidi anachohitaji mkeo ni uwepo wako! Watu kama hawa wanahitaji zaidi watu waliowaamini katika jamii zao!

**36. DULU:** Nuru, mpenzi wangu, ni sawa... Pole sana, Daktari. Ni vile kuwa huyo mtoto ndiye kila kitu… inauma. Nuru amepitia mengi, na kumbe kuna haya... Lakini ni sawa, Nuru… Hakuna tatizo. Sasa hebu lala kidogo. Nitarudi kesho.

**37. NURU:** **(calls out sadly)** Dulu… wewe ndiye mume bora kuliko wanaume wote… Kama si wewe, ningelikufa.

**38. DR. JITO:** Nuru anasema kweli, unajua. Mlimleta wakati unaofaa. Angelikufa kwa sababu ya kuvuja damu. Lakini Dulu, mke wako anakuhitaji sasa. Bado hajatoka katika hatari.

**39. MSIMULIZI:** Nuru Lazima ajipe moyo kwa haya mapigo mawili: dhulma za kingono na kumpoteza mtoto ambaye Dulu alimtaka kwa siku nyingi. Daktari amemhakikishia kuwa atayatibu madhara ya ubakaji. Lakini ataathirika vipi katika hali yake ya matangamano na kihisia? Ati Nuru kweli atahisi yuko salama? Usibanduke. Lakini sasa tujiungeni na Pato, atakapomtembelea mamake Serefa juma hili la mapumziko. Kumekucha kitambo, lakini Pato bado yungaliko kitandani.

**<u>SCENE THREE: PATO AT HOME WITH HER MOTHER SEREFA</u>**

**40. SFX: VILLAGE MORNING ATMO OUTSIDE. BREATHING OF PATO SLEEPING DEEPLY**

**41. SEREFA:** **(surprised)** Pato! Pato! Patooo!

**42. PATO:** **(responds sleepily)** Hmmmm…

**43. SEREFA:** Natumai hujakuwa wakulala hivi kila siku shuleni . Jamani! Ni saa nne sasa na bado ungaliko kitandani! Kwani kumetokea nini? Siku hizi huendi tena mazoezini asubui?

**44. PATO:** Mama, tafadhali niache nilale kidogo. Nimechoka sana.

**45. SEREFA:** Umechoka? **(sarcasm)** Msichana wa miaka 16 ujiweke kama una miaka sitini.

**46. SFX: BLANKET QUICKLY PULLED OFF THE BED**

**47. SEREFA:** Hebu amka – amka na unisaidie kusafisha nyumba. Tunatarajia wageni.

**48. PATO:** **(mumbling)** Sitaki wageni mimi.

**49. SEREFA:** Pato! Unasema nini?

**50. PATO:** **(firmly)** Mama, tafadhali achana na mimi. Si ulisema uliponipeleka kwenye ile shule kuwa nina haki ya kupewa nafasi yangu ya usiri. Basi nahitaji kuwa peke yangu sasa.

**51. SEREFA:** **(shocked)** Aha… vyema… sawa… kama una lazima na hayo. Lakini si mgonjwa wala huna tatizo, sivyo?

**52. PATO:** La.

**53. SEREFA:** Huna jambo?

**54. PATO:** Ndiyo.

**55. SEREFA:** Shuleni pia ni kwema?

**56. SFX: PATO PULLING BLANKET OVER HEAD**

**57. PATO:** **(from under the blanket)** Tafadhali mama, nenda zako nahitaji kulala.

**58. SEREFA:** **(puzzled)** Hujawahi kuwa hivi, Pato. Kama kuna lolote nieleze ili niweze…

**59. PATO:** **(firmly)** Sawa. Kuna jambo unaweza kunisaidia nalo! Niwache nilale!

**60. SEREFA:** **(politely)** Haya, sawa, nakuondokea. Lakini usisahau, mimi bado ni mamako. Kwa hivyo, msichana fanya adabu zako unaponiongelesha sipendi unipandishie sauti.

**61. SFX: DOOR BEING CLOSED**

**62. PATO:** **(starts to cry quietly under the blanket)**

**63. MSIMULIZI:** Mama wengi huona uzito kujuwa matatizo wanayoyapata mabinti zao. Serefa ameshangazwa na tabia za Pato. Lakini kuepuka ubishi; anafikiri tabia za Pato ni kulingana na hali yake ya mabadiliko kutoka usichana hadi uwanawali. Hana habari kwamba Pato anapambana na mambo tofauti: anadhulumiwa kingono na mwalimu wake, Bw. Maneno. Kwengineko, sehemu nyengine ya nchi, Allan hajui afanyeje baada ya kudhulumiwa kingono na jitu analoambiwa ni mjombake, Uncle Joe. Leo mamake Precious ameandaa mlo wa mchana kwa ajili ya wote watatu...

**<u>SCENE FOUR: ALLAN, PRECIOUS NA UNCLE JOE NYUMBANI</u>**

**64. SFX: LUNCH ATMO, RADIO IN BACKGROUND**

**65. ALLAN:** Nimeshiba.

66. **PRECIOUS:** Ati? Allan, hata hujakula!

67. **ALLAN:** Nimeshiba.

68. **JOE:** Sawa, amekuwa kijana mkubwa sasa. Kama hataki kula mwache.

69. **PRECIOUS:** Ndiyo, Joe, najua, hiki ni chakula Allan anachokipenda. Nashangaa hataki kula. Allan, unaumwa? Una hakika hutaki tena chakula?

70. **Silence**

71. **PRECIOUS:** Ala! Allan, nasema na wewe!

72. **ALLAN:** Nataka kwenda kucheza nje…

73. **PRECIOUS:** La. Nilikwambia kuondokea watu mezani wakiwa wanakula ni tabia mbaya.

74. **Silence**

75. **JOE:** Muache nawe. Unamdekeza kama mtoto mchanga.

76. **PRECIOUS:** Lakini ni mtoto mdogo. Ana miaka 10 tu. Tusipomfunza sisi atafunzwa na nani?

77. **JOE:** Allan – nenda.

78. **ALLAN:** Ati?

**79. PRECIOUS:** Huyu mtoto! Husikii? Si ulitaka kwenda, na Joe - namaanisha, Uncle Joe – amekwambia uende.

**80. ALLAN:** Umesema hivyo, Uncle Joe?

**81. JOE:** Ndiyo, Allan. Wewe fanya kile unachotaka. Wanaume waliokamilika hujiamulia watakacho.

**82. SFX: CHAIR BEING DRAGGED SLOWLY**

**83. PRECIOUS:** **(lovingly)** Ati wanaume ndivyo wafanyavyo? Joe, unamharibu mtoto.

**84. JOE:** **(sharply)** Una maana namharibu? Kivipi?

**85. PRECIOUS:** Joe, taratibu, nakutania. Nafurahi kuwa anakusikiliza na kufuata amri zako. Hiyo imekuwa ndoto yangu daima.

**<u>HITIMISHO:</u>**

Mamake Allan, Precious hashuku lolote. Joe anapotabasamu kwa maneno ya mpenziwe, inatufikisha mwisho wa kipindi hiki cha nne, kinachohusu dhulma za kingono barani Afrika. Watatu hawa watafikwa na yapi, Nuru, Pato na Allan? Jiunge nasi katika kipindi kijacho ili kung'amua zaidi. Kwa ajili ya kipindi hiki au kingine kilichopita tembelea wavuti wetu dw.de/lbe. Au tupe maoni yako katika mtandao wetu wa Facebook. Mpaka wakati mwengine: Kwaheri.